

'Taasisi ziwasilishe miradi, mifumo ya Tehama e-GA'

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Morogoro. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imezitaka taasisi za umma kuhakikisha miradi na mifumo yote ya Tehama inayotekelezwa ndani ya taasisi zao inawasilishwa e-GA.

Taasisi hizo zimetakiwa kufanya hivyo wakati wa hatua ya mipango ili kuiwezesha Mamlaka kupitia na kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana mjini hapa na Meneja wa Usimamizi wa Udhhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao, Sultana Seiff alipofunga mafunzo ya siku mbili kwa maafisa Tehama na rasilimali watu kutoka taasisi mbalimbali za umma zilizo katika sekta ya uchukuzi.

Alisema agizo hilo ni utekelezaji

wa matakwa ya kifungu Na. 24 cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 pamoja na kanuni Na.27 ya kanuni za jumla za Serikali Mtandao za mwaka 2020.

"Taasisi zote za umma zinapaswa kuwasilisha taarifa kamili na sahihi za miradi na mifumo yote ya Tehama kupitia tovuti ya huduma za Tehama serikalini (GISP), ili e-GA ifanye mapitio ya miradi hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kibali," alisema Sultana.

Alisema lengo la mamlaka ya Serikali Mtandao ni kuhakikisha taasisi za umma zinatunzia Tehama katika utendaji kazi wake na utoaji wa huduma kwa wananchi.


Alisema kwa kufanya hivyo, huduma hizo zitapatikana kwa wananchi wote kwa wakati kila mahali na kwa wakati na gharama nafuu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Tehama Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Leonard Lwiza alisema ufanisi wa utendaji kazi katika sekta hiyo unategemea ujenzi na uwepo wa mifumo salama na imara ya Tehama.

Hivyo, alisema ni muhimu mifumo hiyo izingatie sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao.

Pia aliwataka maafisa Tehama walioshiriki mafunzo hayo wakawe mawakala wazuri kwa kuhakikisha miradi na mifumo yote ya Tehama katika taasisi zao inazingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao.

Naye Ofisa Rasilimali Watu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Bakari Mbagha aliishukuru e-GA kwa kuandaa mafunzo hayo.



Pamoja na uwepo wa sheria hiyo, mamlaka imeandaa viwango na miongozo ya Serikali Mtandao ambayo taasisi zote za umma zinapaswa kuzingatia katika usimamizi na utekelezaji wa miradi, mifumo na miundombinu ya Tehama."
Sultana Seiff